IJA - WORKERS SACCOS LTD.
Reg. No. TAR 526, P.O.Box 20, Lushoto – Tanga, Tel:+255 (0) 272660133,
Fax: +255 (0)272660021, E-mail: ijaworkerssaccos@gmail.com

# SERA YA UWEKEZAJI

***Imetengenezwa kwa mujibu wa Kifungu cha 74 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika na 6 ya mwaka 2013; na Kanuni namba 84 – 87 za Kanuni za Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo za mwaka 2015.***

CamScanner

# YALIYOMO

DIBAJI ........................................ 1

SEHEMU YA KWANZA ........................................ 2

1. UTANGULIZI ........................................ 2

SEHEMU YA PILI ........................................ 3

2.0 MAENEO MUHIMU YANAYOTAKIWA KUWEPO KATIKA SERA HII ........................................ 3

2.1. Lengo na madhumuni ya shughuli za uwekezaji katika ........................................ Ltd yatakuwa kama ifuatavyo; .3

2.2 Sifa na Ukomo wa uwekezaji ........................................ 3

2.3 Mwanachama kuwa na mamlaka ya kuwekeza ndani ya chama. ........................................ 3

2.4 Sehemu/mahali chama kilipowekeza kwa sasa. ........................................ 3

2.5 Taarifa nyingine muhimu kuhusu uwekezaji wa ........................................ Ltd4

SEHEMU YA TATU ........................................ 4

3.0. MAENEO AMBAYO CHAMA KINATAKIWA KUWEKEZA ........................................ 4

3.1. ........................................ Ltd itawekeza katika maeneo yafuatayo-;4

SEHEMU YA NNE ........................................ 5

4.0 KUIVA KWA UWEKEZAJI NA HATARI ZINAZOWEZA KUJITOKEZA WAKATI WA UWEKEZAJI ........................................ 5

SEHEMU YA TANO ........................................ 6

5.0. UTOAJI WA TAARIFA ZA UWEKEZAJI ........................................ 6

6.0 HITIMISHO ........................................ 6

## *DIBAJI*

*Sera hii ya uwekezaji ya IJA WORKERS' SACCOS LTD imeandaliwa na Bodi ya chama kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 na kanuni za Vyama vya Ushirika wa Akiba na mikopo ya mwaka 2015.*

*Sera hii imeweka mwongozo sahihi wa uwekezaji wa IJA WORKERS' SACCOS LTD kuwekeza katika Taasisi mbalimbali za kifedha kwa kuzingatia kifungu cha 74 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 na Kanuni Na. (84-87 )za Vyama vya Ushirika wa Akiba na mikopo ya mwaka 2015. Bodi na menejimenti wakati wote itawekeza kwa maslahi mapana ya wanachama na chama kwa kuzingatia sera hii.*

*Katika kutekeleza matakwa hayo, sera hii inaweka mwongozo wa kisheria na uwazi katika uwekezaji wa aina mbalimbali utakaofanywa na IJA WORKERS' SACCOS LTD kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 na kanuni za Vyama vya Ushirika wa Akiba na mikopo ya mwaka 2015.*

*Sera hii itatumika wakati wote kama kigezo kikubwa cha kuzingatiwa wakati wakufanya maamuzi ya kifedha na uwekezaji (Financial and investment decisions) kwa maslahi mapana ya wanachama na chama.*

*Sera hii imejumuisha Sehemu tano, **Sehemu ya kwanza** ni utangulizi, **sehemu ya pili ni** maeneo muhimu yanatakiwa katika sera ya uwekezaji, **sehemu ya tatu** ni maeneo ya uwekezaji (Investment destination), **sehemu ya nne** ni Kuiva kwa uwekezaji na hatari zinazoweza kujitokeza wakati wa uwekezaji (Investment maturity and Risks) na **Sehemu ya tano** ni Utoaji wa taarifa za uwekezaji kwa Bodi ya chama (waiver and investment reporting)*



CamScanner

TANZANIA
Registered this......01st......
day of August ......20 2019
.................
Asst. Registrar of Cooperative Societies

## SEHEMU YA KWANZA

### 1. UTANGULIZI

Sera hii ya uwekezaji ya *IJA WORKERS' SACCOS LTD* imeandaliwa na Bodi ya chama kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 na kanuni za Vyama vya Ushirika wa Akiba na mikopo ya mwaka 2015

Sera hii imeweka mwongozo sahihi wa uwekezaji wa *IJA WORKERS' SACCOS LTD* kuwekeza katika Taasisi mbalimbali za kifedha kwa kuzingatia kifungu cha 74 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 na Kanuni Na. (84-87 )za Vyama vya Ushirika wa Akiba na mikopo ya mwaka 2015. Bodi na menejimenti wakati wote itawekeza kwa maslahi mapana ya wanachama na chama kwa kuzingatia sera hii.

Katika kutekeleza matakwa hayo, sera hii inaweka mwongozo wa kisheria na uwazi katika uwekezaji wa aina mbalimbali utakaofanywa na *IJA WORKERS' SACCOS LTD* kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 na kanuni za Vyama vya Ushirika wa Akiba na mikopo ya mwaka 2015.

Sera hii itatumika wakati wote kama kigezo kikubwa cha kuzingatiwa wakati wakufanya maamuzi ya kifedha na uwekezaji (Financial and investment decisions) kwa maslahi mapana ya wanachama na chama.

Sera hii imejumuisha Sehemu tano, Sehemu ya kwanza ni utangulizi, sehemu ya pili ni maeneo muhimu yanatakiwa katika sera ya uwekezaji, sehemu ya tatu ni maeneo ya uwekezaji (Investment destination), sehemu ya nne ni Kuiva kwa uwekezaji na hatari zinazoweza kujitokeza wakati wa uwekezaji (Investment maturity and Risks) na Sehemu ya tano ni Utoaji wa taarifa za uwekezaji kwa Bodi ya chama (waiver and investment reporting)



CamScanner

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MAENEO MUHIMU YANAYOTAKIWA KUWEPO KATIKA SERA

### 2.1. Lengo na madhumuni ya shughuli za uwekezaji katika *IJA WORKERS' SACCOS LTD* yatakuwa kama ifuatavyo;

i. Kuinua mtaji wa chama
ii. Kuinua mtaji wa wanachama
iii. Kupata faida kutokana na uwekezaji husika.
iv. Kupata faida kwa maslahi ya wanachama na chama

### 2.2 Sifa na Ukomo wa uwekezaji

*IJA WORKERS' SACCOS LTD* itawekeza katika uwekezaji usiozidi ***mwaka mmoja***. Umri wa kuiva (matunity) kwa uwekezaji katika chama ni mwaka mmoja tu.

### 2.3 Mwanachama kuwa na mamlaka ya kuwekeza ndani ya chama.

Mwanachama wa *IJA WORKERS' SACCOS LTD* anao uwezo au anaruhusiwa kisheria kuwekeza katika chama chake kwa kuweka Amana, Akiba, au Hisa za hiari. Uwekezaji huu utalipiwa riba maalumu kama itakavyokubalika na kupitishwa na mkutano mkuu wa wanachama wote katika mwaka husika.

### 2.4 Sehemu/mahali chama kilipowekeza kwa sasa.

Chama cha Akiba na mikopo cha *IJA WORKERS' SACCOS LTD* kwa sasa kimewekeza katika maeneo yafuatayo-;

i. Akaunti maalumu (FDR) katika Benki ya ***CRDB PLC*** na ***NMB PLC*** ambapo chama kitajipatia faida ya riba ya asilimia 6% ya fedha zilizowekezwa kwa kipindi cha miezi kumi na mbili(12).

ii. Mikopo mbali mbali iliyokopeshwa kwa wanachama kwa utaratibu maalumu wa sera ya mikopo inayotumika mpaka sasa. Mradi wa Miamala ya Mitandao ya Simu na Miamala ya Kibenki inayofanyika ndani ya jengo la chama.



CamScanner

**2.5 Taarifa nyingine muhimu kuhusu uwekezaji wa *IJA WORKERS' SACCOS LTD***

Bodi ya Uongozi na Menejimenti /watendaji wa *IJA WORKERS' SACCOS LTD* Ltd pamoja na wanachama kwa pamoja tutaendelea kubuni na kuibua aina mbalimbali za uwekezaji wenye faida ndani ya chama na maslahi ya wanachama. Ikumbukwe kwamba uwekezaji wowote utakaobuniwa unatakiwa kufanyika ndani ya miezi kumi na mbili (miezi 12) ''maturity period'' kama kanuni za SACCOS za mwaka 2015 zinavyoelekeza.

## SURA YA TATU

## 3.0. MAENEO AMBAYO CHAMA KINATAKIWA KUWEKEZA

**3.1. *IJA WORKERS' SACCOS LTD* itawekeza katika maeneo yafuatayo-;**

i. Kuweka/ Kuwekeza fedha katika benki kama hatifungati''FDR'' kwa kipindi kisichozidi miezi 12.

ii. Kuwekeza kwenye taasisi nyingine za kifedha na dhamana za serikali kama vile ununuzi wa vipande UTT au hisa katika kampuni zinazofanya vizuri katika soko la fedha (DSE) na dhamana ya serikali ya muda mfupi''treasury bills''

iii. Kuwekeza kwenye SACCOS zilizopata leseni (licenced Saccos) au vyama vya ushirika vya upili (second tier or secondary cooperative societies) ambavyo vimekidhi vigezo kwa mujibu wa sheria na mwongozo wa utoaji wa leseni.

iv. Uwekezaji unaweza kuwa katika mfumo wa MIKOPO ya aina mbalimbali kulingana na sera ya utoaji,ukusanyaji na ufutaji wa mikopo, Akiba, Amana, au Hisa za hiari kwa kuweka riba katika fedha zilizowekwa kama amana.akiba na hisa za hiari kama hazijatumika kama dhamana ya mkopo.

v. *IJA WORKERS' SACCOS LTD* haitawekeza katika mali zisizozalisha (non- earning assets/property/Equipment) kwa kiwango ***kisichozidi asilimia 10 %ya mali zote za chama***. Mali zisizozalisha zitawekezwa kwa asilimia 10% au chini ya asilimia 10%.



CamScanner

vi. Uwekezaji katika ardhi na majengo hautazidi asilimia 5% ya mali zote za chama, kama kanuni Na. 87 (2) inavyoelekeza.

vii. Kabla ya kufanya maamuzi ya kuwekeza, Bodi ya *IJA WORKERS' SACCOS LTD* itafanya upembuzi wa kina na itazingatia mahitaji na hali halisi ya ukwasi na vipindi vya mahitaji makubwa ya mikopo kwa wanachama kama sera ya menejimenti ya ukwasi ,mali na dhima inavyoelekeza.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 KUIVA KWA UWEKEZAJI NA HATARI ZINAZOWEZA KUJITOKEZA WAKATI WA UWEKEZAJI

Katika *IJA WORKERS' SACCOS LTD* yafuatayo yatazingatiwa:-

i. Uwekezaji wowote utakaofanywa utaiva ndani ya mwaka mmoja (one – year – maturity) isipokuwa uwekezaji kama ulioainishwa kwenye sura ya tatu hapo juu.

ii. Chama hakitaweka fedha katika benki moja au taasisi moja ya kifedha kwa kiwango kinachozidi asilimia 25% ya mtaji tete wa chama kwa ajili ya kufanya ''diversification of risks or risks spread''. Hii ni kwa mujibu wa kanuni Na.86 (2) ya SACCOS ya mwaka 2015.

iii. Endapo *IJA WORKERS' SACCOS LTD* itawekeza katika eneo lenye benki moja au taasisi moja tu ya fedha, Mrajis wa Vyama vya Ushirika atatoa idhini ya kuweka fedha zote katika benki au taasisi hiyo moja kulingana na kanuni Na. 86 ya mwaka 2015

iv. Wakati wote *IJA WORKERS' SACCOS LTD* haitawekeza katika maeneo hatarishi ya mtaji wa chama.

v. *IJA WORKERS' SACCOS LTD* itawekeza kwa kusudi la kufikia lengo mahususi (holding to maturity) kulingana na muda wa uwekezaji na mikataba ya uwekezaji itakavyofanyika na kupata ushauri wa kiimandishi kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika kama kanuni Na.76 ya vyama vya Ushirika ya mwaka 2015 inavyoelekeza.



CamScanner

vi. Kila uwekezaji utakuwa na leja yake, ikiainisha aina ya uwekezaji, kiasi, Riba, muda wa kuiva kwa uwekezaji huo, na kuidhinishwa na wajumbe wa Bodi kwa niaba ya mkutano mkuu.

vii. *IJA WORKERS' SACCOS LTD* itatunza kumbukumbu halisi (original copies) zote za uwekezaji katika kasiki ya chama kama sera ya uhifadhi wa kumbukumbu na masharti ya chama yanavyoelekeza.

viii. Mamlaka ya juu kuhusu ridhaa ya uwekezaji wa aina yeyote katika chama, itakuwa ni mkutano mkuu wa wanachama. Bodi ya chama ina wajibu wa kubuni uwekezaji, na kuandika andiko la kuwaelimisha na kuwashawishi wanachama kupitia mkutano mkuu.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0. UTOAJI WA TAARIFA ZA UWEKEZAJI

Wakati wote Menejimenti ya *IJA WORKERS' SACCOS LTD* itatakiwa kutoa taarifa ya uwekezaji kwa Bodi ya chama kila robo mwaka kama kanuni Na.87(1) ikiainisha taarifa zifuatazo-;

i. Aina zote za uwekezaji uliofanywa na chama.

ii. Riba halisi ya kila uwekezaji mpaka siku taarifa hiyo inapotolewa.

iii. Tarehe ya kuiva kwa kila uwekezaji na taarifa nyingine zinazohusiana na kila uwekezaji.

iv. Shughuli za uwekezaji za kila mwezi kama vile kununua na kuuza, na Riba iliyorejeshwa.

v. Malinganisho ya kwenye vitabu (book value) na malinganisho ya soko kwa wakati husika (current market value).

vi. Kuwepo kwa utosherevu wa tengo la uwekezaji (provision for investment loss)

vii. Na taarifa nyingine muhimu kama zipo.

## 6.0 HITIMISHO



CamScanner

Sera hii ya Uwekezaji ya *IJA WORKERS' SACCOS LTD* itafanyiwa marekebisho/mapitio au mabadiliko angalau kila mwaka ili kuboresha jambo/mambo yatakayoonekana yanahitajika kuboreshwa kwa maslahi ya mapana ya chama na wanachama kadiri Bodi ya uongozi na wanachama itakavyoona inafaa kufanya hivyo kama kanuni Na.84(1) inavyoelekeza.

Sera hii ya uwekezaji ya *IJA WORKERS' SACCOS LTD* imeandaliwa na Bodi ya chama na imepitishwa na mkutano mkuu wa wanachama uliofanyika tarehe 03/11/2018. Na kusainiwa na wafuatao;

Jina GEORGE JOSEPH BANDA Wadhifa MWENYEKITI Sahihi ....

Jina IDDI A. MSHANA Wadhifa MAKAMU M/KITI Sahihi ....

Jina SPORA S. NKWABI Wadhifa KATIBU Sahihi ....

Jina MATULO M. MWAKA Wadhifa MJUMBE Sahihi Mwaka

Jina AGNES D. SHIJA Wadhifa MJUMBE Sahihi ....

Jina DAUDI A. HEMBA Wadhifa MJUMBE Sahihi ....

IJA WORKERS' SACCOS LTD.
P. O. BOX 20 LUSHOTO
TAR. 526

Imeidhinishwa na Mrajisi Msaidizi (M) Tanga leo tarehe 01 Mwezi 08 Mwaka 2019

Jina J. SENZIGHE Anuani 5095, TANGA Sahihi ....